TANGAZO LA SERIKALI Na. 798 la tarehe 10/11/2023

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA YA 272)

# AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 29 (d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA LINDI (LINDI WSSA), YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MWAKA, 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi (Lindi WSSA), ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2023.

Marekebisho ya bei

2. Bei za Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi zinarekebishwa kama zilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitakuwa na masharti yafuatayo:

(a) kabla ya kutoa bili ya kwanza yenye bei na ada mpya zilizoidhinishwa, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi itawasilisha ushaidi EWURA wa kuwa imewajulisha wateja wake kuhusu Amri hii na pia imetoa elimu kwa wadau wake ikiwemo wateja, viongozi wa serikali, viongozi wa kisiasa, na wawakilishi wa taasisi za dini juu ya utekelezaji wa Amri ya bei mpya;

(b) ifikapo tarehe 30 Disemba, 2023 au kabla, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira

Lindi itawasilisha EWURA mpango wake wa biashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii;

(c) Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(d) ifikapo tarehe 30 Juni 2024 au kabla, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi itahakikisha kuwa inafikisha huduma ya maji karibu na taasisi za umma ikijumuisha vituo vya afya, zahanati na shule ili kutoa urahisi kwa taasisi hizo kuunganishwa na huduma za maji;

(e) ifikapo ya tarehe 30 Juni, 2025 au kabla, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi itahakikisha inatoa huduma ya maji kwa wakazi wote waishio pembezoni mwa vyanzo vya maji;

(f) Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi itaandaa na kutekeleza mpango wa kutoa elimu kwa wateja wake na kuwasilisha EWURA taarifa ya utekelezaji wa mpango huo kila mwaka;

(g) Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi, itahakikisha inafikia viashiria vya utendaji vilivyoainishwa kwenye Jedwali la Tatu;

(h) Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri hiii na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne;

(i) Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa

zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa mahitaji ya EWURA, ambazo zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Lindi ikilinganishwa na mamlaka nyingine za majisafi na usafi wa mazingira na uboreshaji wa huduma zake; na

(j) kuhakikisha kunakuwepo na huduma endelevu ya maji hususani kipindi cha kiangazi, Mafinga WSSA inapaswa kuandaa na kutekeleza mpango wa kuvuna maji ya mvua.

Kufuta TS Na. 121 la Mwaka 2019 TS Na. 60 la Mwaka 2022

4. Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi (Lindi WSSA), (ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2019 na Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Lindi (Lindi WSSA), ya uondoshwaji na umwagaji wa majitaka (Amri ya Muda) zimefutwa.

## MAJEDWALI

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa

| Kundi la Wateja | Matumizi (m3) | Kipimo | Bei ya Sasa | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 0-5 | Sh./m3 | 1,600 | 2,146 | 2,191 | 2,229 |
| | >5-6 | Sh./m3 | 1,700 | | | |
| | >10 | Sh./m3 | 1,800 | | | |
| Taasisi | | Sh./m3 | 2,100 | 2,575 | 2,629 | 2,675 |
| Biashara | | Sh./m3 | 2,200 | 2,698 | 2,754 | 2,802 |
| Viwanda | | Sh./m3 | 2,200 | 2,698 | 2,754 | 2,802 |
| Magati | | Sh./m3 | 1,500 | 2,000 | 2,000 | 2,000 |
| Wateja wa Jumla | | Sh./m3 | 2,300 | 2,820 | 2,879 | 2,930 |
| Wastani | | Sh./m3 | 1,797 | 2,203 | 2,249 | 2,289 |

1(b): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi kwa Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama Ilivyoelekezwa kwenye Kanuni ya 26 ya Kanuni za Maji za Mwaka 2019 | 26,000 | | |
| Taasisi | | | | |
| Biashara | | | | |
| Viwanda | | | | |

1(c): Ada za Sasa na Zilizoidhinishwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Majumbani | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 40,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 40,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 40,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

1(d): Bei Zilizoidhinishwa za Uondoshwaji Majitaka (Shilingi/Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Ada za Sasa | Ada Zilizopendekezwa | Ada Zinazopendekezwa |
|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24 – 2025/26 | 2023/24 – 2025/26 |
| Majumbani | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Taasisi | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Biashara | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Viwanda | 32,000 | 32,000 | 32,000 |

1 (e): Bei Zilizoidhinishwa za Kumwaga Majitaka (Shilingi/Tripu)

| Aina ya Mteja | Tozo za Sasa | Tozo Zilizopendekezwa | Tozo Zinazopendekezwa |
|---|---|---|---|
| | 2022/23 | 2023/24-2025/26 | 2023/24 – 2025/26 |
| Gari aina zote | 9,000 | 9,000 | 9,000 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(c))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| Maelezo ya Mradi | Gharama (Shilingi) | | |
|---|---|---|---|
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Kununua na kufunga dira za maji 6,000 kwa wateja wapya | 200,000,000 | 200,000,000 | 200,000,000 |
| Kununua na kubadilisha dira za maji 4,191 | 281,100,000 | 105,000,000 | 33,000,000 |
| Kununua Dira 300 za Malipo ya Kabla kwa ajili ya wateja wa Taasisi na Majumbani | 22,800,000 | 33,900,000 | 33,300,000 |
| Kununua vali 138 za milimita 200 kwa ajili ya maeneo 12 | 25,300,000 | 28,000,000 | 28,000,000 |
| Kununua dira za maji kubwa 100 | 25,000,000 | 12,500,000 | 12,500,000 |
| Kukarabati jengo la pampu la Liwayawaya | | 25,000,000 | 25,000,000 |
| Kununua pampu mbili kwa ajili ya kituo cha Liwayawaya | | 50,000,000 | 50,000,000 |
| Kununua kompyuta za mezani 12 na komputa mpakato 8 | 31,152,000 | 6,372,000 | 18,172,000 |
| Kununua pikipiki 10 | 10,400,000 | 10,400,000 | 5,400,000 |
| Kununua gari moja | | | 178,000,000 |
| Kujenga maabara ndogo ya maji | | 90,000,000 | |
| Kununua simu za kiganjani kwa ajili ya matumizi ya ofisi | 900,000 | 2,800,000 | 1,400,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kuongeza mtandao wa maji kwa kilometa 3 eneo na Ngongo | 88,997,513 | | |
| Kutanua mtandao wa maji kwa kilometa 7.9 eneo la Kikwetu | | 230,363,625 | |
| Kutanua mtandao wa maji kwa kilometa 5.3 eneo la Mradi wa Gesi Asilia | | | 287,692,950 |
| JUMLA | 685,649,513 | 794,335,625 | 872,464,950 |

________

JEDWALI LA TATU

________

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(g))*

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Maelezo | Kizio | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Idadi ya Watu Iliyofikiwa na Huduma ya Maji | % | 80 | 90 | 98 |
| Idadi ya Wateja Wapya | Na. | 2,000 | 2,000 | 1,000 |
| Uzalishaji wa Maji | M3 | 1,524,240 | 1,576,800 | 1,646,880 |
| Kiwango cha Upotevu wa Maji | % | 25 | 20 | 20 |
| Ufungaji wa Dira Maji | % | 100 | 100 | 100 |
| Ufanisi wa Ukusanyaji wa Mapato | % | 95 | 97 | 99 |

________

JEDWALI LA NNE

______

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3(h))*

MAHITAJI WA FEDHA YALIYOIDHINISHWA

| Maelezo | Kiasi (Shilingi Milioni) | | |
|---|---|---|---|
| | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
| Gharaza za Uzalishaji wa Maji | 743.30 | 771.29 | 808.20 |
| Gharama za Usambazaji wa Maji | 5.00 | 5.25 | 5.51 |
| Gharama za Huduma ya Majitaka | 6.49 | 6.73 | 7.07 |
| Gharama za Matengenezo | 184.26 | 199.00 | 214.92 |
| Gharama za Wafanyakazi | 725.19 | 884.73 | 909.07 |
| Gharama za Utawala | 242.85 | 255.64 | 264.81 |
| Gharama za Matangazo ya Biashara | 5.90 | 6.16 | 6.43 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Kugharamia Matukio na Misaada | 5.31 | 5.53 | 5.77 |
| Tozo za Benki | 5.41 | 5.77 | 6.13 |
| Jumla ya Gharama za Uendeshaji na Matengenezo | 1,923.72 | 2,140.10 | 2,227.92 |
| Uchakavu wa Miundombinu | 684.70 | 694.67 | 721.94 |
| Uwekezaji | - | 100.00 | 150.00 |
| Jumla ya Mahitaji ya Fedha | 2,608.42 | 2,934.77 | 3,099.86 |
| Ada za Maunganisho Mapya | 52.00 | 52.00 | 26.00 |
| Ada za Kurejesha Huduma kwa Waliokatiwa | 5.00 | 5.00 | 5.00 |
| Tozo za Huduma ya Majitaka | 15.00 | 15.00 | 15.00 |
| Mapato Mengine | 17.49 | 25.36 | 38.03 |
| Mahitaji ya Fedha Kutoka Kwenye Mauzo ya Maji | 2,518.93 | 2,837.41 | 3,015.83 |

Dodoma,
3 Novemba, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*